

TAARIFA KWA UMMA

WITO WA KUKUSANYA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA TANESCO YA KUREKEBISHA BEI ZA UMEME KWA MWAKA 2017

Tarehe 4 October 2016, Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) ilipokea ombi kutoka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) la kutaka kuongeza bei ya umeme kwa wastani wa asilimia 18.19 kwa mwaka 2017. Ombi hili la mabadiliko ya bei ya umeme limewasilishwa kulingana na Agizo la Kubadilisha Bei za Umeme la mwaka 2016 lililoanza kutumika tarehe 1 Aprili 2016 ambalo liliagiza TANESCO iwasilishe ombi la mabadiliko ya bei ya umeme kwa mwaka 2017.

Kwa mujibu wa kifungu Na. 19(2)(b) cha Sheria ya EWURA, Sura Na. 414, kutakuwa na Mikutano ya Taftishi ili kupata maoni toka kwa wadau ikiwa ni pamoja na Baraza la Ushauri la Serikali (GCC), Baraza la Ushauri la Watumia Huduma Zinazodhibitiwa na EWURA (CCC) na wananchi wote kwa ujumla, kuhusu uhalali wa bei zinazopendekezwa. Mikutano ya taftishi itafanyika katika mikoa ya **Mwanza, Mbeya, Arusha na Dodoma** siku ya **Jumatano, tarehe 16 Novemba 2016** na siku ya **Jumatano, tarehe 23 Novemba 2016** jijini Dar es Salaam kuanzia saa **3:30 asubuhi**. Umma utajulishwa hapo baadaye mahali ambapo mikutano husika itafanyika.

Wadau wanaopenda kutoa maoni kwa maandishi wanaombwa kufanya hivyo kwa kutuma maoni yao kwa Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kwa anuani iliyoonesha hapo juu ndani ya kipindi cha hadi kufikia tarehe **25 Novemba 2016**. Maelezo zaidi kuhusu ombi husika yanapatikana katika tovuti ya EWURA, www.ewura.go.tz au kwa kuandika barua kwa Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kwa kutumia anuani inayoonekana hapo juu.

Imetolewa na:

Mkurugenzi Mkuu,

Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA)

4 Novemba 2016